

JAMHURI YA MUUNGANO TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



Kumb. Na. AR/ILAVING/B/44/24/FRC

Tarehe: 17/01/2023

Mkurugenzi Mtendaji,
Kituo cha Uwekezaji Tanzania,
S.L.P 938,
DAR ES SALAAM.



YAH: UMILIKI WA KIWANJA NA. P 27955 ENEO LA VINGUNGUTI - ILALA

Husika na kichwa cha habari hapo juu, pia rejea barua yako ya tarehe 09/01/2023 yenye Kumb. Na. PP.10/042628/10.

2. Awali kiwanja hiki kilikuwa namba 2036 Kitalu "B" Vingunguti ambacho kilikuwa kinamilikiwa na TANZANIA PASTA INDUSTRIES LIMITED kwa Hati iliyosajiliwa kwa namba 136883. Waliomba kurejesha Hati hiyo baada ya kununua maeneo mengine ya pembeni ili waweze kupima upya na kuunganisha eneo moja.
3. Taratibu za kuandaa Mchoro wa Mipangomiji namba TPD No: 1/651/690 zilikamilika na ukafanyika upimaji wa eneo hili na kupata Ramani iliyosajiliwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani kwa namba ya Usajili DSMS0027848 na kuwa kiwanja namba P 27955 Vingunguti.
4. PASTA INDUSTRIES TANZANIA LIMITED waliomba kumilikishwa na ofisi yetu ilibaini kuwa hisa kubwa ni kwa wamiliki wa kigeni na kuwashauri kuwasilisha maombi yao kwanza katika ofisi yako ili watambulike kama wawekezaji na kumilikishwa kwa mujibu wa sheria za uwekezaji.
5. Kwa barua hii na kulingana na kumbukumbu zetu eneo la kiwanja hiki linamilikiwa na PASTA INDUSTRIES TANZANIA LIMITED.
6. Tunashukuru kwa Ushirikiano.

Farida R. Chambulilo

Kny: MKURUGENZI WA JIJI LA DAR ES SALAAM

OFISI YA MKURUGENZI, 1 MTAU WA MISSION, S.L.P 20950, 11883 DAR ES SALAAM, SIMU NA 2128800,
2128805, Tovuti: www.dcc.go.tz, Barua Pepe: info@ilalamc.go.tz